Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imejizatiti kuhakikisha kwamba inafikia malengo yaliyoko kwenye Dira ya Maendeleo ya Taifa na kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2020-2025.

TCRA itaendelea kuimarisha usimamizi, kuhimiza watoa huduma kufikia Watanzania wengi zaidi na kujiandaa kupokea teknolojia mpya za mawasiliano.

Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Dkt. Faustine Ndugulile akipewa maelezo kuhusu mfumo wa kufuatilia maudhui ya utangazaji wakati alipotembelea TCRA Desemba 2020. Alifuatana na Naibu Waziri, Mhe. Mhandisi Kundo Andrew Mathew na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dr. Zainab Chaula.

Kanuni kutatua kero za vifurushi

Mhandisi James Kilaba, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania,

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kama Mdhibiti wa sekta ya Mawasiliano ya Kieletroniki na Posta nchini, pamoja na mambo mengine, ina majukumu ya kusimamia gharama na tozo katika huduma za mawasiliano zinazotolewa na watoa huduma.

Katika kutekeleza majukumu yake TCRA inachukua hatua mbalimbali kuhakikisha kwamba mahitaji ya wadau wa pande zote (Serikali, watoa huduma na watumiaji wa huduma) yanafikiwa kupitia huduma husika.

Kwa mfano, TCRA imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ikihusisha watoa huduma ili kushusha bei ya simu za kawaida (basic tariffs), ambazo ni bei za nje ya vifurushi.

Hii ni baada ya kuona kuwa jitihada za kushusha bei za muingiliano (interconnection charges) zilizokokotolewa na kuanza kutumika mwaka 2018 hazikuakisiwa kwenye bei za nje ya vifurushi.

Kwa kulinganisha mwaka 2018 na Feb 2021, wastani wa bei za kupiga simu ndani ya mtandao pasipo kujiunga na kifurushi zimeshuka kutoka TZS. 290.27 kwa dakika hadi TZS. 70.81 kwa dakika, sawa na punguzo la asilimia 76. Bei za kupiga simu kutoka mtandao mmoja kwenda mtandao mwingine bila kujiunga na kifurushi nazo zimeshuka kwa wastani kutoka TZS. 387.55 kwa dakika hadi TZS. 71.99 kwa dakika, sawa na punguzo la asilimia 81. Bei za kutuma ujumbe mfupi (SMS) zimeshuka kutoka TZS. 64.12 hadi TZS. 22.23 kwa SMS, sawa na punguzo la asilimia 65.

Wastani wa bei za data kwa Mb moja bila kujiunga na kifurushi zimeshuka kutoka TZS. 104.86 kwa Mb moja mpaka TZS. 24.16 kwa Mb sawa na punguzo la asilimia 77.

Madhumuni makubwa ya juhudi hizi yalikuwa ni kupunguza tofauti kubwa iliyokuwepo kati ya bei za vifurushi na zile za kutumia huduma bila kujiunga na vifurushi.

Pamoja na jitihada hizi, bado TCRA iliendelea kufuatilia kwa ukaribu suala la vifurushi, kutokana na ukweli kwamba asilimia zaidi ya 90 ya watumiaji wa huduma za mawasiliano wanatumia vifurushi.

Pia kulikuwa na malalamiko mengi juu ya vifurushi, hasa kwenye matumizi ya data, ikiwemo kutumika kwa salio kuu pale kifurushi kinapofikia ukomo wa matumizi.

Mwezi Novemba 2018, TCRA ilitoa maelekezo kwa watoa huduma kuwa:-

1. Simu zote za sauti kwenye vifurushi ziwe zinahesabiwa au kulipiwa kwa sekunde zilizotumika; na kiwango cha chini cha hesabu kiwe ni sekunde.

2. Huduma za data kwenye vifurushi zihesabiwe kwa kiwango cha kilobaiti 10; na kiwango kidogo cha kutozwa kwa data pia kiwe ni kilobaiti 10.

3. Watoa huduma waweke utaratibu unaomuwezesha mteja anayejiunga na huduma za vifurushi kuchagua na kukubali kutozwa gharama zisizokuwa kwenye vifurushi mara muda wa kifurushi alichojiunga nacho au uniti za kifurushi husika kumalizika; na endapo mteja hatachagua, basi asikatwe kwenye salio lake.

4. Makadirio na kiwango cha chini cha uniti zinazoweza kutozwa/kulipiwa kifahamike na kupatikana kwa wateja ili waweze kufanya maamuzi sahihi.

   Pamoja na maelekezo hayo, TCRA ilijiridhisha juu ya umuhimu wa kutengeneza utaratibu ambao kwa kiwango kikubwa utatatua kero za vifurushi.

   Katika kutengeneza utaratibu huo, tarehe 5 Februari, 2021, TCRA ilitoa matangazo ya kukaribisha maoni ya wadau wote kuhusu huduma ya vifurushi vinavyouzwa na watoa huduma ili kuhakikisha kuwepo kwa ufanisi na kuwezesha upatikanaji wa huduma bora kulingana na thamani ya malipo yaliyofanywa na wanaojiunga na vifurushi husika.

   Kama itakavyokumbukwa, kimsingi mashauriano haya yalilenga kupata majibu katika maeneo 10 yafuatayo:-

   i. Kuunganishwa moja kwa moja kifurushi (auto renewal) mara baada ya kifurushi alicholipia Mteja kufikia ukomo wa muda wa matumizi au kinapoisha;

   ii. Kuunganisha watumiaji kwenye vifurushi bila ridhaa yao, ikiwa ni pamoja na kutokuwepo kwa ridhaa ya kutumia taarifa za mtumiaji;

   iii. Kutokuwepo uwazi katika makato ya huduma ya data wakati wa kutumia vifurushi;

   iv. Malalamiko ya watumiaji juu ya kumalizika kwa kasi kwa vifurushi vya data;

   v. Matangazo ya huduma yanayopotosha na vigezo na masharti visivyo bayana;

   vi. Watumiaji kujikuta wanatozwa gharama kubwa mara tu kifurushi kinapoisha kutokana na kukatwa, bila ridhaa yao, salio lao lililolipiwa kabla ya huduma;

   vii. Uelewa wa watumiaji kuhusu huduma na bidhaa kwenye vifurushi;

   viii. Watumiaji kupoteza muda wa maongezi, idadi ya meseji (SMS) au data ambazo walikuwa hawajazitumia baada ya kumalizika/ukomo wa muda wa kifurushi;

   ix. Mashaka kwamba gharama za baadhi ya huduma zinafidiwa kwa kuuza data kwa vifurushi chini ya gharama halisi; na

   x. Kuwa na kanuni ndogo zinazohusu huduma ya vifurushi na kuzitofautisha na promosheni na ofa maalum.

Jumla ya maoni 3,278 yalipokelewa kutoka kwa wadau mbalimbali ikijumuisha watumiaji, watoa huduma na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

TCRA inawashukuru sana wote waliotoa maoni na ushauri kwa lengo la kuboresha huduma hizi za vifurushi hapa Tanzania.

Kwa kuzingatia maoni na ushauri wa wadau hao, TCRA imeweza kuandaa Kanuni ndogo ambazo zitawezesha kutatua kero za watumiaji wa huduma na kuongeza ustawi wa Sekta ya mawasiliano.

Utekelezaji wa hizi kanuni ndogo utaanza rasmi tarehe 02 Aprili, 2021 na tunaamini utaendelea kujibu mambo mengi yanayolalamikiwa na watumiaji kwa sasa.

Baadhi ya mambo yaliyomo katika Kanuni ndogo hizo yameainishwa katika toleo hili.

Mashauriano vifurushi yaleta mrejesho chanya

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imepokea na kuchakata maoni na mapendekezo 3,278 njia za kuboresha utoaji wa huduma za vifurushi vya mawasiliano.

Mapema mwaka huu TCRA ilisambaza waraka wa mashauriano na wadau kuhusu vifurushi na kukaribisha maoni na mapendekezo.

Hatua hii ilifuatia kuwepo kwa malalamiko mengi kutoka kwa watumiaji na wadau wengine kuhusu namna vifurushi vya huduma za mawasiliano vinavyopangwa na kutolewa kwa watumiaji. Malalamiko pia yalihusu namna huduma za vifurushi zinavyopangwa na kuwekwa kwenye matangazo ya huduma na ofa maalum kutoka kwa watoa huduma.

Mamlaka ilitambua masuala ambayo yanatakiwa kushughulikiwa ili kuboresha muitikio wa watumiaji, kushawishi matumizi ya huduma za mawasiliano ya simu, kuongeza uhakiki wa mapato kutokana na matumizi, kuhimiza uwazi katika kutoza gharama za matumizi na kuhakikisha ufanisi na kuwezesha upatikanaji wa huduma bora kulingana na malipo yaliyofanywa na aliyejiunga na vifurushi husika.

TCRA ilianzisha mashauriano ya umma ili kupata maoni kutoka kwa watumiaji na wadau kuhusu kuwepo kwa mfumo muafaka wa kusimamia uwekaji wa vifurushi vya huduma za mawasiliano ya simu zinavyotolewa hivi sasa na gharama zinazoambatana navyo (gharama na tozo za vifurushi).

Mashauriano haya yalilenga kuanzisha mfumo wa usimamizi kwa utoaji wa huduma za mawasiliano ya simu kwa utaratibu wa vifurushi.

Kifurushi cha huduma za mawasiliano ya simu kinaamanisha mchanganyiko wa huduma kama vile muda wa maongezi kwa dakika, data, ujumbe mfupi (SMS) ambavyo vinauzwa kama kitu kimoja. Vifurushi hivi vinatolewa kwa njia mbili, ambazo ni: kama kifurushi kamili ambacho watumiaji wanaweza kununua tu kama huduma ya kifurushi husika au kifurushi mseto ambavhio kinatoa fursa kwa watumiaji kununua ama kifurushi chote kwa (kawaida) bei pungufu au kununua huduma tofauti za kifurushi hicho.

Soko la mawasiliano ya simu Tanzania lina ushindani, ikimaanisha kwamba watoa huduma za mawasiliano ya simu kadhaa wanatoa huduma kwa kushindana na watoa huduma wengine katika eneo husika la matumizi. Upangaji na utoaji wa vifurushi kama mkakati vinatumiwa na watoa huduma wote kuongeza mapato, kubakiza na kuongeza watumiaji wa huduma na kuridhisha watumiaji wao. Vifurushi vikitolewa kwa bei pungufu vinaongeza ustawi wa watumiaji kwa kuongeza matumizi yao ya huduma.

Ingawaje nadharia ya kiuchumi ya kupanga na kutoa vifurushi inaongeza thamani kwa watoa huduma, watumiaji na uchumi kwa ujumla, ni rahisi kwa mafanikio haya kutoweka iwapo vifurushi hivi vinatolewa bila kuvifuatilia kabisa. Katika muktadha wa sheria ya ushindani, upangaji na utoaji wa vifurushi bila usimamizi unaweza kushusha ubora wa huduma na pia kushawishi na kuchochea mwenendo unaopingana na ushindani ikiwa ni pamoja na utoaji wa huduma chini ya gharama za uzalishaji. Hii inaweza kuleta madhara kwa maendeleo ya sekta.

Masuala muhimu yaliyotakiwa kushughulikiwa katika mapendekezo ya mwongozo wa vifurushi, utangazaji wa huduma na ofa maalum; na kwa maana hiyo msingi wa masuahuriano kwa wadau yalikuwa :-

a) Kuunganisha upya moja kwa moja vifurushi vilivyolipiwa kwa matumizi ya mara moja mara tu vinapoisha.

b) Kuunganisha watumiaji kwenye vifurushi bila ridhaa yao, ikiwa ni pamoja na kutokuwepo kwa ridhaa ya kutumia taarifa za mtumiaji.

c) Kutokuwepo uwazi katika matumizi ya data wakati wa kutumia vifurushi.

d) Kupungua ubora wa huduma ikiwa ni pamoja na kukatika kwa simu katikati ya mazungumzo na msongamano katika mtandao.

e) Malalamiko ya watumiaji kuhusu kutozwa kuliko viwango vilivyowekwa, kutokana na kupungua kwa kasi kwa vifurushi vya data.

f) Matangazo ya huduma yanayopotosha na vigezo na masharti visivyoeleweka.

g) Mshangao wa watumiaji kujikuta wanatozwa gharama kubwa kutokana na kukatwa kwa salio lao lililolipiwa kabla ya huduma bila ridhaa yao mara tu kifurushi kinapoisha.

h) Uelewa wa watumiaji kuhusu huduma na bidhaa kwenye vifurushi.

i) Watumiaji kujikuta wakipoteza uniti (units) ambazo watakuwa hawajazitumia baada ya kumalizika kwa muda wa kifurushi.

j) Mashaka kwamba gharama za baadhi ya huduma zinafidiwa kwa kuuza data kwa vifurushi chini ya gharama halisi.

TCRA ilitambua kwamba masuala haya ni ya msingi na yalihitaji hatua za haraka za udhibiti. Masuala ya mashauriano yalihusu:

1. **Muda wa kutangaza huduma, ofa na huduma za vifurushi:**

Hili lilitokna na lengo ;a Mamlaka kuweka muda wa chini na wa juu kabisa na ukubwa wa chini na wa juu kabisa wa vifurushi (idadi ya uniti za huduma) vikiwa vimeunganishwa na vipindi vya matumizi na kuweka muda wa chini kabisa wa vifurushi kutumika/kumalizika muda.

Maoni yalitakiwa kuhusu muda wa chini na wa juu kabisa wa matumizi ya kifurushi na ukubwa wa chini na wa juu kabisa wa kifurushi.

2. **Masuala ya gharama na tozo zinazohusu kutozwa zaidi, kuunganishwa kwenye huduma ambayo haitolewi au kumalizika kwa ghafla kwa uniti za vifurushi:**

Kutozwa zaidi ni mojawapo ya malalamiko yanayopokelewa mara nyingi. Kuna wakati watumiaji wamelalamikia kutozwa bila kupatiwa

kiasi cha huduma walizonunua au vifurushi walivyojiunga navyo kumalizika ghafla na bila kutokana na matumizi halisi.

Maoni yalikusanjwa kuhusu utaratibu wa kuwafidia watumiaji ambao wamethibitishwa kwamba wametozwa zaidi.

3. **Kuunganishwa bila ridhaa ya mtumiaji:**

Ili kupunguza matukio ambamo watumiaji wanaunganishwa kwenye huduma TCRA inatarajia kuweka usawa na viwango ambavyo watoa huduma watatakiwa kuzingatia wanapowaunganisha au kuwaondoa watumiaji kwenye huduma. Baadhi ya watoa huduma wanatumia ujumbe unaojitokeza kwenye simu za watumiaji kuwasilisha taarifa za kuunganishwa au kuwaondoa watumiaji kwenye huduma na wakati mwingine kufuatia ujumbe huo mtumiaji moja kwa moja anabebeshwa mzigo wa kujiondoa yeye mwenyewe kutoka kwenye huduma husika.

Maoni yalikusanywa kuhusu mfumo wa kuwezesha kufikisha ujumbe kwa njia itakayohakikisha uwazi, kuondoa mzigo kwa watumiaji na kuhifadhi ushahidi wa kujiunga.

4. **Kutokuwepo usawa katika kupata huduma kwenye vifurushi:**

Watumiaji wanapata huduma za mitandao tofauti kwa kutumia namba tofauti na njia za kujiunga na huduma. Ingawaje hali hii inawezesha kutofautisha huduma, kwa kiasi

fulani kinamchanganya mtumiaji na kuongeza gharama wakati watumiaji watakapotaka kuhama kutoka mtandao mmoja kwenda mwingine ama kwa kubadilisha laini ya simu au kutumia Huduma za Kuhamia Mtandao Mwingine na kubaki na namba zao, yaani Mobile Number Portability.

TCRA ilitaka maoni kuhusu kuwepo kwa namba moja itakayotumiwa na wote kupata taarifa kuhusu vifurushi na huduma nyingine ambazo zinafanana kwa mitandao yote.

5. **Vipimo vitakavyotumika kufuatilia huduma na bidhaa kwenye vifurushi:**

Ili kuhakikisha kwamba huduma bora zinatolewa kwa watumiaji na kuzihakiki kwa usahihi, TCRA inapendekeza kuanzishwa kwa vipimo vitakavyokuwa vigezo vya kupima usahihi wa tozo na gharama.

Watumiaji na wadau wengine walitoa maoni yao kuhusu vigezo vya vipimo na tofauti ambazo zinaruhusiwa/zinakubalika wakati wa kuhakiki matumizi halisi kulinganisha na uniti zilizonunuliwa au mtumiaji alizolipia alipojiunga ili haya yazingatiwe wakati wa kuchukua hatua za kiusimamizi.

6. **Vigezo na Masharti visivyoeleweka na vinavyohadaa (matangazo ya kupotosha ya huduma):** Hili lilitokana na kuwepo malalamiko mengi kuhusu vigezo na masharti visivyoeleweka wakati wa kutangaza huduma na ofa maalum, na ukweli kwamba wengi wa wanaojiunga na huduma hawana uelewa kamili wa huduma zilizoko kwenye vifurushi ni suala jingine.

Watumiaji waliulizwa iwapo wanasoma kwa kina na kuelewa vigezo na masharti ya kifurushi kaba ya kununua na iwapo Vigezo na masharti vilivyowekwa vilieleweka na vinatoa taarifa zote zinazohitajika kufanya uamuzi wenye mantiki. Aidha walitakuwa kutaja vigezo na masharti kwenye kifurushi, matangazo ya huduma na ofa maalum ambavyo walidhani haviko wazi na vinaleta mkanganyiko na vinatakiwa kuondolewa/kuwa revised mara moja.

7. **Idadi ya vifurushi na aina wanazoweza kuchagua watumiaji:**

Wakati wa mashauriano kulikuwa na vifurushi vipatavyo 754 vinavyotolewa na watoa huduma wote. Vifurushi vya chini kwa kila mtoa huduma ni 24 wakati vya juu kabisa ni 294, ambavyo vimepangwa kwa siku, wiki, mwezi, siku 90 au 180. Ingawaje taarifa hii inaweza kutolewa kwa watumiaji wa simu zenye uwezo wa juu (smart phones) kwa kutumia Graphic User Interface (GUI) kwenye program rununu (app), taarifa hizi zinasumbua zinapowasilishwa kwa njia ya meseji ya maandishi hasa kwa watumiaji wenye simu za kawaida. Kulikuwa na maswali manne kwenye kipengele hiki.

- Je kuwe na kiwango cha mwisho cha idadi ya vifurushi ambavyo ni rahisi kupatikana na kupitiwa na mtumiaji kabla ya kuamua kujiunga?

- Nini mapendekezo ya idadi ya vifurushi kwa kila mtoa huduma?

- Kifurushi kiendelee kutumika kwa muda gani kabla ya kuboreshwa (kurekebisha bei au kiasi cha uniti katika kifurushi)?

- njia ipi bora ya kuwasilisha kwa mtumiaji gharama za matumizi ya vifurushi na taarifa za Vigezo na Masharti kuhusiana navyo?

Muda wa kurudiwa matangazo, ofa maalum na kubadili gharama vifurushi:

Hili lilitokana na kusudio la Mamlaka kuainisha idadi ya matangazo ya huduma, ofa maalum na na mabadiliko ya gharama za vifurushi ili kutokuwachanganya watumiaji hadi waishie kuchagua kile wasichokuwa wamekusudia.

Maoni yalitakiwa kuhusu idadi muafaka ya matangazo ya huduma na ofa maalum kwa watumiaji na muda wa kurudia matangazo ya huduma na ofa maalum kwa watumiaji.

Uelewa wa matumizi ya vifurushi:

Wadau walitakiwa kutoa maoni kuhusu kutolewa notisi bila malipo kwa watumiaji wanaolipa baada ya kuduma na wanaolipa kabla huduma kuwekwa kwa kuonyesha asilimia iliyotumika au uniti za kifurushi zilizobakia. Kwa maneno mengine watumaji wapewe taarifa kwa vipindi vifurushi vikifikia asilimia 90 na 100 ya kumalizika kwa kifurushi au kwamba wapewe taarifa za huduma zilizobakia (muda wa maongezi, meseji na data) lakini watahadharishwe angalau mara mbili kabla ya asimilia 100 ya matumizi ili wawe na muda wa kutosha kufanya uamuzi na kuchukua hatua za watakachochagua.

Kumalizika kwa vifurushi na kuendeleza vifurushi visivyotumika:

Kuendeleza vifurushi vya data baada ya kumalizika kwa muda wa matumizi yake ni eneo ambalo limelalamikiwa sana na wengi. Mamlaka ilipendekeza kuendeleza matumizi ya data ambazo hazikutumika katika muda wa kifurushi. Maswali yaliulizwa kwenye maneo manne:

• Athari za uamuzi huu kwenye kupanga bei na matumizi ya huduma za mawasiliano ya simu.

• Maoni kuhusu kuwepo kwa vifurushi ambavyo havina muda wa kumalizika.

• Mapendekezo, ikiwa ni pamoja na Vigezo na Masharti ya kuendeleza matumizi ya data ambazo hazikutumika katika muda wa kifurushi.

• Mapendekezo ikiwa ni pamoja na Vigezo na Masharti ya kuhamisha data kutoka mtumiaji mmoja kwenda mwingine katika mtandao huohuo.

Kuwepo kwa Sera ya matumizi yenye usawa kuwawezesha watumiaji kuwa na taarifa muhimu kusimamia na kufutilia matumizi:

Kwa upande wa kuwepo kwa Sera ya matumizi yenye usawa kuhusiana na utangazaji wa huduma, ofa na vifurushi; wadau waliulizwa kuhusu mambo ya kuzingatia wakati wa kutoa sera bora ya matumizi yenye usawa kwa watumiaji ili waweze kuendelea kuwezeshwa kufanya uamuzi baada ya kuwa na taarifa muhimu.

Wadau walitakiwa kupendekeza viwango vya sera ya matumizi yenye usawa kuhusiana na matumizi ya vifurushi.

Baada ya kuchambua maoni ya wadau,ilionekana kwamba kwamba asilimia kubwa walitaka:

1. Muda wa chini wa vifurushi uwe masaa 24.

2. Muda wa juu wa ofa na huduma za vifurushi uwe mwezi mmoja.

3. Kuwepo mfumo utakaowezwesha watumiaji waliothibitishwa kutozwa zaidi kurudishiwa kiasi walichotozwa.

4. Uhakiki wa utozaji na matumizi ya uniti katika kifurushi ufanyike kupitia kumbukumbu za matumizi.

5. Huduma za vifurushi ikatwe mara kifurushi husika kinapomalizika.

6. Mtumiaji ambaye kifurushi alichojiunga kimemalizika na hajajiunga huduma za ziada aweze kutuma ujumbe wa *"tafadhali nipigie"* na aweze kupiga simu za dharura.

7. Kuwepo namba moja itakayotumiwa na watumiaji wote kupata taarifa kuhusu vifurushi na huduma nyingine ambazo zinafanana kwa mitandao yote.

8. Kuwe na jina moja litakalotumika kwa watoa huduma wote kwa vifurushi visivyokuwa na muda wa mwisho wa matumizi.

9. Vigezo na masharti viwekwe kwa namna ambayo itaeleweka na taarifa zote zinazohitajika kufanya uamuzi wenye mantiki zitolewe.

10. Vigezo na masharti vitolewe kwa ufupi na kwa njia itakayofanya vieleweke kirahisi.

11. Ubora wa huduma uongezwe.

12. Kuwe na kiwango cha mwisho cha idadi ya vifurushi ambavyo ni rahisi kupatikana na kupitiwa na mtumiaji kabla ya kuamua kujiunga na kimojawapo.

13. Kila mtoa huduma awe na vifurushi chini ya vitano (5).

14. Kusiwe na mipaka ya muda wa vifurushi kuendelea kutumika kabla ya kuboreshwa (kurekebisha bei au kiasi cha uniti katika kifurushi).

15. SMS zitumike kuwasilisha kwa mtumiaji gharama za matumizi ya vifurushi na taarifa za vigezo na masharti kuhusiana navyo.

16. Taarifa ya matumizi zitolewe mara kwa mara kwa ujumbe mfupi wa maandishi (SMS) na mtumiaji atumie kumbukumbu hizo kujua taarifa ya matumizi ya kifurushi husika.

17. Idadi ya matangazo ya huduma na ofa maalum kwa watumiaji ipunguzwe.

18. Idadi ya marudio ya matangazo ya huduma na ofa maalum kwa watumiaji itegemee huduma husika.

19. Watumiaji wapewe taarifa ya kumalizika kifurushi mara mbili vikifikia asilimia 90 na 100 ya matumizi.

20. Kuwe na vifurushi ambavyo havina muda wa kumalizika.

21. Vifurushi visivyotumika vipelekwe mbele na viendelee kutumika.

22. Kuwe na utaratibu wa kuhamisha data kutoka mtumiaji mmoja kwenda mwingine katika mtandao huohuo.

Uelewa muhimu kufurahia vifurushi

Watumiaji wa huduma za mawasiliano wamekuwa na hoja na maswali kuhusiana na kulazimishwa kutumia kifurushi usiku, simu 'kitochi' kuunganishwa na data, vifurushi kumalizika kabla ya muda na gharama za vifurushi. Ufafanuzi TCRA kutokana na kanuni mpya za vifurushi kwa baadhi ya hoja za watumiaji kuhusiana na huduma za vifurushi ni kama ifuatavyo.

1. **Kulazimishwa kutumia kifurushi usiku:**

   Mtoa huduma yeyote yule hamlazimishi mteja wake kutumia kifurushi usiku.

   Mteja anachagua na kujiunga na kifurushi katika vile vinavyotolewa na mtoa huduma kutokana na mahitaji ya mtumiaji, muda wa matumizi na uwezo wake wa kifedha.

   Kwa kujiunga na kifurushi mteja anakubali kupewa huduma aliyoinunua kwa muda uliowekwa.

   Mtoa huduma anaweka vifurushi vya usiku ambavyo ni nafuu sana usiku kwa sababu mtandao wake hautumiki sana kipindi hicho na hivyo kuwa na uwezo wa kutoa uniti nyingi kwa wale watumiaji wa usiku.

2. **Simu za 'kitochi' kuunganishwa na data:**

   Kimsingi mtoa huduma anapanga vifurushi mbalimbali kulingana na mahitaji ya wateja, akiwa anajua kabisa kuwa kuna wenye simu za vitochi na wenye simu za uwezo mkubwa (simu janja).

   Kuna vifurushi vya dakika za maongezi na ujumbe mfupi tu na vipo vya muda wa maongezi tu. Vifurushi hivi ni mahususi kwa wenye simu za 'kitochi'.

   Mteja anachagua na kujiunga na kifurushi kutokana na mahitaji yake, uwezo wa kifedha, na uwezo wa kifaa chake cha mawasiliano.

   Mtumiaji wa huduma anashauriwa kusoma na kuchagua kifurushi kinachoendana na uwezo wa simu yake au kifaa chake cha mawasiliano.

3. **Vifurushi kumalizika muda**

   Vifurushi vyote havipaswi kumalizika muda. Kitu pekee ambacho kinapaswa kumaliza kifurushi kinatakiwa kiwe ni mtumiaji kuongea hadi dakika zake ziishe au kukitumia hadi uniti ziishe.

   Kimsingi, Kwa kujiunga na kifurushi mteja anakubali kupewa huduma aliyoinunua kwa muda uliowekwa. Kwa kawaida, vifurushi hivi haviwezi kutumika baada ya muda uliowekwa kwisha hata kama havijatumika.

   Ili kumlinda mteja, maboresho yaliyofanyika ni pamoja na:-

   - Mtoa huduma kumwezesha mtumiaji wa huduma kuhamisha uniti za kifurushi kwenda kwa watumiaji wasiozidi wawili ndani ya mtandao wake.

   - Mtoa huduma kumwezesha aliyejiunga na kifurushi chochote kuendelea kutumia uniti za kifurushi ambazo zitakuwa zimesalia ndani ya muda wa matumizi uliowekwa kwa kununua tena kifurushi hicho hicho kabla ya kumalizika kwa muda wake.

4. Nini kimefanyika kuhusiana na vifurushi kwisha kabla ya muda. Kwenye simu za sauti, kila mtumiaji anapopiga simu anapewa taarifa kuhusu muda aliotumia kwa maongezi, na anaweza kulinganisha kiasi cha muda alionunua na aliopewa. Pia mtumiaji anaweza kuangalia salio na kupata ujumbe mfupi kuhusu matumizi ya kifurushi chake.

   Data ni eneo linalolalamikiwa sana; ambapo mtumiaji hawezi kupata taarifa kila data inapotumika. TCRA imelishughulikia suala hili kwa namna mbili:-

   i. Kanuni ndogo zimewataka watoa huduma kuweka program rununu

   ii. (mobile app) itakayowawezesha watumiaji wa data kufuatilia matumizi yao ya data (mtumiaji wa data mwenye simu ya uwezo mkubwa (simu janja).

   iii. TCRA imeandaa mwongozo kwa watumiaji kuhusu mfumo wa uendeshaji (Operating system) wa simu janja pamoja na programu rununu zinazotumiwa na watumiaji wa data kupata huduma mbalimbali.

Kanuni ndogo za Vifurushi

Kanuni Ndogo za Gharama za Tozo za Vifurushi, Utangazaji Huduma na Ofa Maalum, ambazo zitaanza kutumika tarehe 2 Aprili 2021 zina vipengele vifuatavyo:

Mwenye leseni hatatoa huduma za vifurushi bila kibali cha Mamlaka.

Huduma za vifurushi zitakazotolewa zitapangwa katika makundi ya (a) Chini ya masaa 24, (b) Siku, (c) Wiki, (d) Mwezi, (e) zaidi ya mwezi na (f) vifurushi visivyokuwa na mwisho wa muda wa matumizi.

Mwenye leseni atahakikisha kwamba taarifa za vifurushi vyote vilivyoidhinishwa na Mamlaka zinapatikana kwenye tovuti zao kwa Kiingereza na Kiswahili na kwamba zinachapishwa kwenye gazeti linalosambazwa maeneo mengi zaidi.

Mtoa huduma atahakikisha kwamba bei za vifurushi zinazingatia bei husika ya chini na ya juu zilizowekwa na Mamlaka.

Watoa huduma hawatakuwa na vifurushi zaidi ya 50 kwa wakati mmoja vyenye mchanganyiko wa huduma zinazotolewa kwa watumiaji (muda wa maongezi, data au SMS) kwenye maeneo wanayotoa huduma isipokuwa vifurushi vya kimataifa na wanaotumia mitandao ya nyumbani wakiwa nchi nyingine.

Vifurushi vinavyotolewa kwa watumiaji havitaondolewa, havitarekebishwa au kubadilishwa ndani ya miezi mitatu baada ya kuidhinishwa.

Watoa huduma watatumia istilahi rahisi na vigezo na masharti yaliyo wazi kuhusu vifurushi vinavyotolewa, ikiwa ni pamoja na maelezo ya kina kuhusu huduma husika na maeneo yote ambayo huduma zinapatikana, watumiaji wanaostahili huduma hizo, kasi ya kupakia au kupakua data.

Mabadiliko yoyote kwenye vifurushi vilivyoidhinishwa yatahusu tu watumiaji watakaojiunga na huduma husika baada ya mabadiliko na kwamba hayataathiri watumiaji waliojiunga kwenye huduma hizo kabla ya mabadiliko hayo.

Wenye leseni watatoa fursa kwa watumiaji wa huduma za mawasiliano kuchagua na kujiunga na vifurushi visivyokuwa na ukomo wa muda wa matumizi vitakavyo patikana kwenye menyu kuu na watatumia jina linalofanana kwa vifurushi hivi ili vitambulike kwa wepesi.

Majukumu ya kutoa taarifa za matumizi ya kifurushi

Kila mwenye leseni atatoa taarifa ya matumizi wakati kila matumizi ya kifurushi yakifikia asilimia 50, 80 na 100 kwa vifurushi vya muda wa maongezi, data na SMS.

Mwenye leseni ataweka mfumo wa kumwezesha mtumiaji wa huduma mwenye simu janja kufuatilia matumizi yake ya data kwa kupakua program rununi (app) ya mtoa huduma.

Mwenye leseni ataweka utaratibu unaowawezesha wanaojiunga na huduma za vifurushi kuchagua na kukubali kutozwa gharama zisizokuwa kwenye vifurushi mara muda wa vifurushi waliojiunga navyo au uniti za kifurushi husika kumalizika. Utaratibu huu wa kuchagua na kukubali utakuwa chaguo msingi mpaka pale anayejiunga achague na kukubali kutumia gharama nje ya kifurushi.

Wenye Leseni watakuwa na utaratibu wa kuwawezesha waliojiunga na vifurushi kuendelea kutumia muda au uniti za vifurushi ambazo zitakuwa hazijamalizika ndani ya muda wa matumizi uliowekwa kwa kuzingatia ununuzi wa kifurushi hicho hicho kabla ya kumalizika kwa muda wake.

Watoa huduma watakahikisha huduma za vifurushi zinazingatia gharama halisi za utoaji huduma kwa namna ambayo itawezesha kutoza gharama zenye uhalisia kwa kila huduma ndani kifurushi husika.

Mwenye leseni hatafanya matangazo zaidi ya matatu au kutoa ofa maalum zaidi ya tatu kwa wakati mmoja kupitia maongezi, SMS na data.

Promosheni na Ofa Maalum

Kutangaza huduma na ofa maalum kutakuwa hivi:

a) Muda uelezwe waziwazi;

b) Kuwe na muda wa chini wa mwezi mmoja na muda wa juu usiozidi miezi mitatu; na

c) Yasirudiwe kabla ya kumalizika miezi mitatu

Mwenye leseni ataweka vigezo na masharti vilivyo wazi kuhusu utangazaji wa huduma na ofa maalum.

Mfumo wa uendeshaji wa simu zenye uwezo mkubwa

Simu yako yenye uwezo mkubwa, au simu janja kama zinavyotambulika ni kifaa cha thamani na chenye matumizi mengi. Kukifanya cha kisasa kwa kuweka mifumo ya kisasa zaidi ya uendeshaji ni sehemu muhimu ya kuhakikisha kwamba kinaendelea kukuwezesha kukitumia kwa ufanisi wa juu zaidi.

Kusasisha mfumo wa uendeshaji wa simu zenye uwezo mkubwa, unapojulishwa kufanya hivyo, kunasaidia kuziba mianya ya kiusalama na kuboresha uwezo wa jumla wa kifaa husika. Hata hivyo, kuna hatua za kuchukua kabla ya kufanya hivyo ili kulinda kifaa chako na picha zozote au mafaili binafsi yaliyohifadhiwa ndani yake.

Kabla ya kusasisha mfumo wa uendeshaji

Kabla ya kuanza kusasisha au kuinua kiwango cha kifaa, chukua hatua chache zitakazosaidia kuepuka matatizo:

- **Chaji simu yako:** Epuka hali ya simu yako kuwa na chaji ndogo wakati wa kusasisha kwa kuhakikisha kwamba kifaa kina angalau asilimia 70 ya chaji.

- **Cheleza (back up) mafaili yako:** Usasishaji na uboreshaji wa mfumo wa uendeshaji havitakiwi kuathiri data zilizohifadhiwa kwenye simu yako ya uwezo mkubwa, lakini kucheleza mafaili ni jambo jema ili data ziwe salama.

- **Hakikisha kifaa chako kinatangamana na uboreshaji wa mfumo wa uendeshaji:** Mfumo mpya wa uendeshaji unaweza usiwe umetengenezwa kwa vifaa vyote vya zamani zaidi.

- **Futa programu rununu (apps) ambazo huzitumii tena:** Mfumo mpya wa uendeshaji unaweza kuhitaji kiasi kikubwa cha kumbukumbu ya kifaa chako. Futa apps ambazo zinachukua tu nafasi.

- **Angalia kifurushi chako kilichobakia na kiasi cha data zinazotakiwa kusasisha mfumo wa uendeshaji:** Hakikisha kwamba una kifurushi cha data cha kutosha kwa usasishaji/uboreshaji wa mfumo wa uendeshaji kwani bila data za kutosha kifurushi kitamalizika na usasishaji na uboreshaji havitafanikiwa.

Baada ya kusasisha mfumo wa uendeshaji wa simu yako

Wakati mwingine mfumo mpya wa uendeshaji utakuwa na mipangilio iliyowekwa wakati wa utengenezaji ambao ni tofauti na mpangilio uliochagua na utajitokeza moja kwa moja kwenye mpangilio mpya badala ya wa zamani. Baada ya kuweka mfumo mpya wa uendeshaji kuna mipangilio ambayo unatakiwa kuhakiki kuhakikisha kwamba simu yako haijiendeshi au kutumia data kwa namna usiyotaka.

- Angalia kwa makini mpangilio wa Wi-Fi: Simu nyingi zenye uwezo mkubwa zinaweza kukuhamishia moja kwa moja kwenye mpango wako wa matumizi ya data wakati muunganisho kwenye Wi-Fi ni hafifu. Hali hii ikiendelea inaweza kusababisha matumizi ya data wakati usiotegemea. Amua iwapo unataka kuwasha au kuzima mfumo unaowezesha matumizi ya data.

- **Angalia kwa makini usasishaji wa moja kwa moja wa data, ambao wakati mwingine unajitokeza chini ya mpangilio wa matumizi ya data:** Iwapo utazima mfumo unaowezesha matumizi ya data, programu rununu zinaweza kusasishwa tu kwa kutumia maunganisho ya Wi-Fi. Hii inaweza kusaidia kuzuia matumizi makubwa ya data, hasa kwa programu rununu ambazo hutumiii mara kwa mara.

- **Angalia kwa makini mpangilio unaowezesha faragha ya matumizi ya kifaa chako na muunganisho kwenye mitandao:** Hakikisha kwamba huduma za kutambua mahali ulipo, uwezo wa vifaa kuunganishwa kupitia Bluetooth, kufuatilia apps na mpangilio ya mitandao ya kijamii vimewekwa kwa mpangilio na upendeleo kama unavyotaka.

- **Angalia kwa makini ulinganifu wa mfumo wa uendeshaji na apps zako muhimu:** Wakati mwingine mfumo mpya wa uendeshaji unaweza usitangamane na mojawapo ya apps zako zilizopo hadi ziunganishwe. Hakikisha kwamba kifaa chako kinatangamana na mfumo wa uendeshaji unaoboreshwa. Inawezekana mfumo mpya wa uendeshaji haukutengenezwa kwa ajili ya vifaa vya zamani kidogo. Angalia kwa makini kuona usasishaji wa apps zozote ambazo hazifanyi kazi vizuri. Vilevile, unaweza kuwasiliana na watengenezaji wa kifaa au mtoa huduma kubadilishana taarifa za mwitikio wa ulinganifu wa apps. Angalia taarifa za namna ya kuwasiliana naye kwenye hati za malipo, kwenye kifaa chako au mtandaoni.

Kituo cha Huduma kwa Watumiaji

Kwa maelezo zaidi kuhusu masuala ya watumiaji, tembelea Kituo cha Huduma kwa Watumiaji cha TCRA kilichopo ghorofa ya kwanza ya jengo la Mawasiliano Towers, Barabara ya Sam Nujoma Dar es Salaam.

Mikakati endelevu kuinusuru Posta

Na Lokila Mosso

Idadi ya vitu vinavyosafirishwa na Posta ya taifa imepungua kwa zaidi ya mara sita ndani ya miaka mitano na mara mbili katika muda wa mwaka mmoja, hali ambayo imeibua haja ya kuwa na mikakati endelevu ya kuendelea huduma kwenye sekta hii.

Takwimu za mawasiliano zinaonyesha kwamba idadi ya vitu vilivyosafirishwa mwaka 2020 ilikuwa 5,140,440 kulinganisha na 12,153,541 mwaka 2019 na 31,259,171 mwaka 2015

Huduma za posta zimeathiriwa hivi karibuni na kuzuka kwa janga la homa kali ya mapafu inayoletwa na virusi vya UVIKO-19 na hatua zilizofuatia za kupunguza shughuli za kijamii na kibiashara za kila siku, ikiwemo baadhi ya nchi kuweka karantini, hivyo kupunguza shughuli za biashara zinazohusu matumizi ya huduma za posta. Aidha kupungua safari za ndege kati ya mataifa kumechangia hali hii.

Athari za UVIKO-19 kwa sekta ya Posta zimekuja wakati huduma za usafirishaji wa barua na vifurushi na malipo kupitia Posta zikiwa zimeathiriwa na ukuaji wa kasi wa teknolojia ya habari na mawasiliano na matumizi yake.

Aidha, baadhi ya huduma za usafirishaji wa vifurushi na vipeto zinatolewa na kampuni zenye leseni za kutoa huduma hizo kimataifa, Afrika Mashariki, ndani ya Tanzania, kwenye miji na kati ya miji. Leseni kwa mabasi ya abiria yanayosafirisha

vifurushi zimeongezeka mara tatu kati ya 2015 na 2020, takwimu za sekta kwa mwezi Desemba 2020 zinaonyesha. Posta ya Taifa inakabiliana na ushindani kwenye eneo hili la huduma.

Baadhi ya watoa huduma za Posta wamechukua hatua mbalimbali kukabiliana na kushuka kwa biashara ikiwa ni pamoja na kuboresha huduma kwa wateja na kutumia teknolojia kutoa huduma mbalimbali.

Umoja wa Posta Afrika, wenye makao yake makuu Arusha umezitaka taasisi za Posta katika Bara hili kubuni mikakati endelevu ya kukabiliana na changamoto zinazojitokeza.

"Katika hali ya sintofahamu kutokana na kuzuka kwa janga la UVIKO-19 tunatarajia sekta ya Posta ulimwenguni kwa ujumla na hasa Afrika kuendelea kuweka mikakati endelevu ya kuendelea kutoa huduma", anaandika Katibu Mkuu wa PAPU, Bwana Younouss Djibrine katika ujumbe wake wa kumbukumbu ya kuanzishwa Umoja huo, tarehe 18 Januari mwaka huu. (Tafadhali rejea ukurasa wa nne (4) sehemu ya Kiingereza ya toleo hili – Mhariri).

Kwa upande mwingine takwimu za Desemba 2020 zinaonyesha ongezeko kubwa la huduma za simu za mkononi ikiwa ni pamoja na kuongeeka kwa kiasi kikubwa kwa laini za simu, akaunti za pesa kupitia simu na idadi ya ving'amuzi vya televisheni.

Jedwali: Huduma na watoa huduma (2015-2020)					
2015	2016	2017	2018	2019	2020
Idadi ya watoa huduma za Posta na kusafirisha vifurushi na vipeto					
36	33	35	28	92	119
Idadi ya vitu vilivyosafirishwa na Posta					
31,259,171	12,098,784	10,121,388	10,829,272	12,153,541	5,140,440
Idadi ya akaunti za pesa kupitia simu za mkononi					
17,939,349	18,080,622	21,889,618	23,367,826	25,864,318	32,268,630
Idadi ya watumiaji wa intaneti					
17,263,523	19,862,525	22,995,109	23,142,960	25,794,560	28,470,506
Idadi ya steheni za redio					
106	148	156	158	183	193
Idadi ya vituo vya televisheni					
31	31	33	36	43	50
Idadi ya ving'amuzi vinavyotumika					
910,395	1,062,128	2,078,353	2,611,617	2,525,289	2,814,003
Rejea: https://www.tcra.go.tz/statistic/2015%20Quarterly%20Statistics%20Reports/december					

TCRA strategic goal, quality policy

The Tanzania Communications Regulatory Authority has the duty of enhancing the welfare of Tanzanians by promoting effffective competition and economic effifficiency; protecting the interests of consumers and protecting the fifinancial viability of effifficient suppliers. TCRA is also responsible for promoting the availability of regulated services to all consumers, including low income, rural and disadvantaged consumers; enhancing public knowledge, awareness and understanding of the regulated sectors and protecting and preserving the environment.

Strategic goal

"To enhance the welfare of Tanzanians through effffective and effifficient regulation that promote innovation and ensure universal access to secure, quality and affffordable communication services".

Objectives

1. To modernize TCRA operations by enhancing staffff competences, quality research on regulated services and utilizing state of the art technologies;

2. To promote effifficient, reliable and secure communications infrastructure and applications;

3. To promote effifficient and affffordable communications services and increase access to Postal and ICTs in underserved and un-served areas;

4. To protect interests of stakeholders and enhance awareness of their rights and obligations;

5. monitor performance of regulated services and enforce compliance to legislation, regulations and standards;

6. To coordinate implementation of National, Regional and International Sector commitments.

Quality Policy

Tanzania Communications Regulatory Authority is committed to achieve its strategic goal and ensure customer satisfaction through Quality Management System.

Quality Objectives

1. Improved quality processes and procedures in the regulation of the communication sector.

2. Achieved high level of customer satisfaction in accordance with TCRA's Client Service Charter.

3. Maintained compliance with relevant statutory and regulatory requirements.

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

ISO 9001:2015 CERTIFIED

ISO 9001:2015 CERTIFIED

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania(TCRA) ni taasisi ya Serikali inayosimamia sekta ya mawasiliano. TCRA ilianzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Na. 12 ya 2003. TCRA ina viwango vya ISO 9001:2015.

Maeneo yanayosimamiwa

Mitandao ya simu na intaneti, masafa ya mawasiliano,huduma za Posta na usarishaji wa vipeto katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na huduma za utangazaji (kama vile redio na televisheni) kwa Tanzania Bara tu. Zanzibar ina Tume inayosimamia utangazaji.

Kazi za TCRA

- Kutoa leseni, kuongeza muda wa leseni na kufuta leseni
- Kuweka viwango kwa bidhaa na huduma zinazosimamiwa
- Kuweka viwango vya kanuni na masharti ya kusambaza bidhaa na huduma zinazosimamiwa
- Kudhibiti viwango na bei
- Kufuatilia utendaji wa sekta ya mawasiliano kuhusiana na viwango vya uwekezaji; upatikanaji wa huduma, ubora na viwango vya huduma; gharama za huduma; ufanisi wa bidhaa na usambazaji wa huduma.
- Kufanikisha utatuzi wa malalamiko na migogoro baina ya watoa huduma na kati ya mtoa huduma na mtumiaji wa huduma.
- Kufanya kazi na kutekeleza majukumu mengine kwa mujibu wa sheria husika
- Kusambaza taarifa kuhusu mambo ambayo ni muhimu kwa ajili ya shughuli za Mamlaka.

TCRA na ustawi wa Watanzania

Katika kufanya kazi zake, Mamlaka inajitahidi kuendeleza ustawi wa jamii ya Tanzania kwa:-
- Kukuza ushindani unaofaa na ufanisi wa uchumi
- Kuendeleza upatikanaji wa huduma zilizodhibitiwa kwa watumiaji wote ikiwa ni pamoja na wenye kipato kidogo waliopo vijijini na wateja walio katika mazingira magumu.
- Kulinda maslahi ya watumiaji
- Kuendeleza elimu kwa wananchi kuhusu utambuzi na uelewa wa sekta zilizodhibitiwa ikiwa ni pamoja na haki na wajibu wa watumiaji;namna ambavyo malalamiko yanaweza kuwasilishwa na kutatuliwa na kuhusu majukumu, kazi na shughuli za Mamlaka.